

"HAKUNA USINGIZI MNONO BILA MKESHA"

12 Septemba, 2020



Ukiweza kulala usingizi fofofo na kuamka siku inayofuata ukiwa salama salimini wewe pamoja na mali zako, jua kuna watu walikesha kulinda usalama wako.

Ukurasa 1

Kuna makundi au vikundi vya watu wanadharau mkesha huo kwa kudhani hawahitaji kulindwa, wanajilinda wenyewe.

Hata kama una walinzi wanyumba na jiko pamoja na silaha za moto; benki unayotunzia fedha za kuwalipa walinzi wako inalindwa na wewe? Soko linalokupa mahitaji ya maisha yako? Miundombinu unayotumia? Hospitali unayotibiwa na familia yako? Anga? Mtandao? Mtaa wenu? Dhamana zako? Shule na vyuo? Ofisi za umma na binafsi zinazotoa huduma kwa jamii? Mikesha inaendelea maeneo hayo ndiyo sababu waweza pata utulivu wa kulala usingizi fofofo.

Lakini hata wale wenzangu na mimi tusiomiliki 'assets' tunapaswa kuthamini ulinzi wa utu wetu, maisha yetu na huduma zetu. Wanaokesha, wanazingatia hilo kwetu sote.

Ulinzi wa watu hauishii nje ya mwili wa binadamu tu, bali unatakiwa ufike hadi ndani ya mwili wako. Jipime mwenyewe; uliwahi kulala usingizi fofofo ukiwa kwenye majanga au madhira yoyote? Mfano; Unaugua au kuuguza? Mwizi anavunja nyumba yako kwa bahati ukaweza kushtuka toka usingizini, ukafanikiwa kumkurupusha mwizi huyo, vipi utaweza kulala tena

usingizi fofofo? Nyumba ya jirani yako inaungua moto, ukasema, "sio yangu, acha nilale!" Na mengine mengi. Natumaini hakuna kulala hapo.

Sasa basi, ina maana ukiona umelala vizuri na kuamka salama, kuna watu walikesha au wanakesha kuhakikisha kila kitu au watu wanakuwa salama na wala hawabugudhiwi na mtu yeyote. Pia kudhibiti majanga yasitokee nakukudhuru. Mfano halisi ni Tanesco, ingawa wameweka mitambo yao kwa weledi mkubwa lakini wanakikosi kinakesha kuchukua tahadhari na kuhakikisha huduma bora inapatikana usiku na mchana.

Alikadhalika kuwa na uwezo wa kujikimu kwako, huo ni mkeshwa wa watu fulani. Wanafikiria, kwa namna gani wataweza kukufanya uweze kupata kipato angalau usishindwe kujitafutia riziki ya siku (chakula au malazi) hata kama kisitoshe na kuridhisha.

Sasa kuna mtu anaamka toka usingizini kitu cha kwanza kufanya nikuandika matusi mtandaoni. Au kusimama jukwaani na kuanza kuporomosha matusi. Vijana tubadilike, tuanze kukesha tukipanga mbinu za kutokomezwa umasikini tulionao badala ya kulala ili

tuamke, kutukana matusi na kukejeri watu na mafanikio ya watu waliokesha.

Pongezi ziwafikie majeshi yote Tanzania Bara na Visiwani na wale wote wanaokesha kwa ajili yetu, tunaowajua na tusiowajua pia.

Pongezi nyingine ni kwa wale watendaji wetu katika idara mbalimbali wanaojitolea kukesha kwa ajili yetu. Hata wanaokesha kutuletea nyanya sokoni au kuchoma vitumbua ili tukiamka tukute mambo bambam! Mwenyezi Mungu awalinde.